

# HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSEGA

(Barua zote zipelekwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)

MKOA WA SIMIYU

Tel : 0282 981193

Fax : 0282 981194

Email : dedbusega@yahoo.com



Sanduku la Posta 157,  
BUSEGA.

KUMB.NA.BDC/S.20/10/50

Tarehe : 23 Februari, 2018

## TANGAZO LA KAZI

**MKURUGENZI MTENDAJI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSEGA ANAPENDA KUWATANGAZIA WATANZANIA WOTE WENYE SIFA NA NIA YA KUFANYA KAZI KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSEGA KUOMBA NAFASI IFUATAYO:**

### **1. MTEKNOLOJIA MSAIDIZI-MAABARA TGHS A. NAFASI 1**

#### **a. Sifa ya mwombaji:**

- Awe na Elimu ya Kidato cha nne (IV) au sita (VI)
- Awe na cheti kwenye fani ya mteknolojia maabara msaidizi (NTA LEVEL 5) kutoka chuo kinachotambulika na serikali.
- Awe na cheti cha usajili kutoka bodi ya usajili wa wataalamu wa maabara.
- Awe na Umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 40.

#### **b. Kazi na Majukumu**

##### **Mteknolojia Msaidizi -Maabara**

- i. Kuandaa vitenganishi (reagents) vya kufanyia vipimo vya maabara
- ii. Kufanya kazi za awali sampuli zinazoletwa maabara
- iii. Kukusanya damu kutoka kwa wagonjwa na watu wanaojitolea
- iv. Kurekodi matokeo ya vipimo kwenye rejista
- v. Kutayarisha vifaa vya kazi
- vi. Kuhifadhi kwa mujibu wa taratibu sampuli zote zinazohitaji kuhifadhiwa baada ya uchunguzi
- vii. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake.

**MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIWA KWA WAOMBAJI WOTE  
WENYE SIFA NI HAYA YAFUATAYO:-**

- a. Maombi yatumwe kwa;  
Mkurugenzi Mtendaji (W),  
Halmashauri ya Wilaya  
S.L.P. 157,  
**BUSEGA.**
- b. Barua za maombi ziambatane na wasifu binafsi (CV) nakala ya vyeti vya Elimu, Taaluma na cheti cha kuzaliwa. Vyeti vyote vithibitishwe na Hakimu au wakili wa Serikali.
- c. Asiwe aliacha, kuachishwa au kufukuzwa kazi kwenye Utumishi wa Umma.
- d. Aambatishe picha moja aliyopiga hivi karibuni (Passport size) na iwe ya rangi
- e. Walioajiriwa wapitishwe barua zao kwa waajiri wao wa sasa
- f. Barua zote ziandikwe kwa mkono zikiwa na anwani ya mwombaji na namba ya simu kama ipo.
- g. Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe **03 MACHI, 2018**

Imetolewa na

**MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA  
S.L.P. 157,  
BUSEGA.**

**MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA  
HALMASHAURI YAWILAYA  
BUSEGA**